**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

***Simu*: +255-26-2323189**

***Barua pepe*: ps@moha.go.tz**

***Tovuti*: www.moha.go.tz**

**Mji wa Serikali - Mtumba,**

**Mtaa wa Habari/Afya**

**S. L. P. 2916,**

**40483 DODOMA.**

**26 Aprili 2025**

## TAARIFA KWA UMMA

## MSAMAHA WA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KWA WAFUNGWA KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 61 YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 26 APRILI, 2025

Tarehe 26 Aprili, 2025 Taifa letu linaadhimisha Miaka 61 ya Muungano wa Tanzania. Katika kuadhimisha tukio hili, Mheshimiwa Rais ametumia mamlaka aliyopewa chini ya Ibara ya 45(1) (a) – (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutoa msamaha kwa wafungwa.

**Msamaha huu umewahusu wafungwa wa makundi mbalimbali kama ifuatavyo: -**

(i) Wafungwa wote wapunguziwe moja ya sita ($^{1}/6$) ya vifungo vyao wanavyovitumikia hivi sasa pamoja na punguzo la kawaida la moja ya tatu ($^{1}/_{3}$) linalotolewa chini ya kifungu cha 49(1) cha Sheria ya Magereza Sura ya 58. Wafungwa hao sharti wawe wamehukumiwa kifungo cha miaka miwili (2) na kuendelea na wawe wameingia gerezani kabla ya tarehe 02 Machi, 2025 isipokuwa wafungwa walioorodheshwa katika sharti la 2(i – xii);

(ii) Wafungwa wagonjwa wenye magonjwa ya kudumu au sugu ambao wapo kwenye hatua ya mwisho (Terminal Stage) na ugonjwa huo uthibitishwe na jopo la Waganga chini ya uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya;

(iii) Wafungwa wote waliohukumiwa na mahakama kutumikia vifungo vya maisha gerezani wabadilishiwe vifungo vyao na kuwa vifungo vya miaka thelathini (30) kuanzia tarehe ya hukumu na hawatapata punguzo la $^{1}/_{3}$. Wafungwa hao wawe wamekaa gerezani miaka mitano (5) na kuendelea kuanzia tarehe ya hukumu;

(iv) Wafungwa wa kunyongwa waliomaliza taratibu za kimahakama wabadilishiwe adhabu ya kifo na kuwa kifungo cha maisha;

(v) Wafungwa waliobadilishiwa adhabu ya kifo kwa msamaha wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka adhabu ya kifo na kuwa kifungo cha maisha gerezani wabadilishiwe adhabu ya kifungo cha maisha na kuwa Kifungo cha miaka thelathini (30) gerezani na hawatapata punguzo la $^{1}/_{3}$;

(vi) Wafungwa wazee wenye umri wa miaka sabini (70) au zaidi ambao wamehukumiwa kifungo cha muda maalum/ukomo na waliokaa gerezani kwa muda wa miaka miwili (2) na kuendelea. Umri huo uthibitishwe na jopo la Waganga chini ya Uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa Wilaya;

(vii) Wafungwa wa kike walioingia na mimba gerezani au wenye watoto wanaonyonya;

(viii) Wafungwa wenye ulemavu wa mwili na afya ya akili wasio na uwezo wa kufanya kazi. Ulemavu huo uthibitishwe na jopo la Waganga chini ya Uenyekiti wa Mganga Mkuu wa Mkoa/Mganga Mkuu wa

Wilaya;

(ix) Wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini (Under Presidential Pleasure) ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 10 au zaidi;

(x) Wafungwa wa kike wenye Watoto wasionyonyesha walioko gerezani; na

(xi) Wafungwa wenye ulemevu wa akili.

**Aidha, Msamaha huo haujawahusu wafungwa wafuatao:-**

(i) Wafungwa wanaotumikia vifungo chini ya Sheria ya Bodi za Parole Sura ya 400 (R.E 2002), Sheria ya Huduma kwa Jamii Sura ya 291 (R.E 2002) na Kanuni za Kifungo cha Nje {*The Prisons (Extra Mural Penal Employment) Regulations, 1968*} pamoja na waliowahi kukiuka masharti chini ya sheria hizo na kurudishwa gerezani kutumikia adhabu zao;

(ii) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani kwa makosa ya uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, rushwa na usafirishaji au kujihusisha kwa namna yoyote ile na madawa ya kulevya ikiwemo bangi;

(iii) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani kwa makosa ya utekaji au wizi wa watoto, kupoka, kuwapa mimba wanafunzi na makosa yote yanayohusiana na ukatili dhidi ya watoto na kujihusisha kwa namna yoyote ile na biashara haramu ya binadamu;

(iv) Wafungwa waliopatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo gerezani kwa makosa ya kukutwa na viungo vya binadamu, unyanganyi,

unyang'anyi wa kutumia nguvu, unyang'anyi wa kutumia silaha, kumiliki silaha, risasi, milipuko au kujaribu kutenda makosa hayo;

(v) Wafungwa wanaotumikia kifungo gerezani kwa makosa ya kujihusisha kwa namna yoyote ile na nyara za Serikali au ujangili;

(vi) Wafungwa wanaotumikia kifungo gerezani kwa makosa ya wizi/ubadhilifu wa fedha za Serikali;

(vii) Wafungwa wanaotumikia kifungo gerezani kwa makosa ya kutoroka au kujaribu kutoroka chini ya ulinzi halali au kusaidia kutendeka kwa makosa hayo;

(viii) Wafungwa wenye makosa ya kuua watoto wachanga, ugaidi, uharamia na makosa ya kimtandao, (Infanticide, Terrorism, Piracy And Cyber Crimes);

(ix) Wafungwa wanaotumikia kifungo cha pili na warudiaji;

(x) Wafungwa waliowahi kupata Msamaha wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isipokuwa kwa wafungwa waliobadilishiwa adhabu kutoka adhabu ya kunyongwa na kuwa kifungo cha maisha gerezani na waliobadilishiwa adhabu kutoka kifungo cha maisha na kuwa kifungo cha kawaida;

(xi) Wafungwa waliotenda makosa ya kinidhamu gerezani ambao makosa hayo hayajatimiza mwaka mmoja (1) mpaka kufikia tarehe 26 Aprili, 2025;

(xii) Wafungwa wa madeni (Civil Prisoners).

Wafungwa elfu nne mia nane themanini na saba **(4,887)** wamenufaika na msamaha huu ambapo arobaini na mbili **(42)** kati yao wanaachiliwa huru tarehe 26 Aprili, 2025 na elfu nne mia nane arobaini

na tano **(4,845)** wanabaki gerezani kumalizia sehemu ya kifungo kilichobaki baada ya kupewa msamaha huu. Ni matarajio ya Serikali kuwa wafungwa hao watarejea tena katika jamii kushirikiana nawananchi wenzao katika ujenzi wa Taifa letu na kwamba watajiepusha kutenda makosa ili wasirejee tena gerezani.

**<u>WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI</u>**

**26 APRILI, 2025**